# SALAMU ZA MTENDAJI MKUU WA OSHA, BI. KHADIJA MWENDA, KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI, APRILI 28, 2024- JIJINI ARUSHA.

**Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko** (MB), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na waalikwa wote mliojumuika nasi hapa.

Ninawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania….

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**; awali ya yote napenda kumshukuru Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutujalia afya njema na kwa neema na baraka zake imempendeza kutukutanisha hapa leo kwenye kilele cha maadhimisho ya siku hii ya Usalama na Afya mahali pa kazi Duniani.

Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa Mgeni Rasmi pamoja na majukumu mazito ya kitaifa uliyonayo, lakini kwa kutambua na kuthamini shughuli hii, umekubali kuwa nasi leo katika maadhimisho haya, nakushukuru sana na karibu sana.

Kadhalika, naomba niwashukuru Wadau wetu wa Utatu katika usimamizi wa masuala ya Usalama na Afya kazini ambao ni TUCTA na ATE bila kusahau Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kushirikiana nasi bega kwa bega katika maandalizi ya maadhimisho haya, kipekee kabisa naomba nimshukuru Mkurugenzi Mkazi wa ILO Kanda ya Afrika Mashariki, **Ndugu Caroline Khamati Mugalla,** kwa namna ambavyo yeye binafsi na ofisi yake imekuwa ikitupatia ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yetu  ikiwemo kufadhili maadhimisho haya jambo ambalo limepelekea Taasisi yetu kufanikiwa kutimiza malengo yake.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**; pamoja na shukrani hizo, kazi yangu hapa ni kukutambulisha wageni mbali mbali waliopata fursa ya kujumuika nasi katika maadhimisho haya yanayofanyika kitaifa hapa Jijini Arusha. Hivyo, kwa heshimana na taadhima, naomba utambue uwepo wa wageni wafuatao;

- Mhe. Patrobas Katambi (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu).
- Mhe.Fecilian Gasper Mtahengerwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. Paul Christian Makonda.
- Mhe. Thomas Ole Sabaya, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Arusha.
- Bi. Edith Simtengu, Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala akimwakilisha Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu).
- Ndugu Missaile Albano Musa, Katibu Tawala Mkoa wa Arusha;
- Dkt. Adelhelm Meru, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri OSHA.
- Bi. Caroline Khamati Mugalla, Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO);
- Ndugu Jaffary Ally, akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Waajiri Nchini (ATE) na Mjumbe wa Bodi ATE.
- Comred Juliana Mpanduji, Katibu wa Chama cha Wafanyakazi Sekta ya Mawasiliano, akimwakilisha rais (r ndogo) wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA).
- Dkt John Mduma, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF);
- Bi. Lulu Mengele Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii NSSF.
- Ndugu Vonnessi Koka, Meneja wa PSSSF Kanda ya Kaskazini akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF.

- Ndugu Usekelege Mpulla Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA);
- Bi.Lilian Denis, Mwakilishi wa Kamishna wa Kazi na Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya OSHA.
- Wakurugenzi Ofisi ya Waziri Mkuu- Kazi,Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu;
- Wakurugenzi Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi,Vijana,Ajira na Wenye Ulemavu.
- Wakurugenzi kutoka Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA);
- Watumishi wote kutoka Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA);
- Washiriki wote wa Maonesho ya siku ya Usalama na Afya Duniani.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**; hawa ni baadhi ya viongozi walioweza kufika hapa kushirikiana nasi katika maadhimisho haya ya siku ya Usalama na AfyaDuniani. Nami kwa niaba menejimenti na watumishi wa OSHA naomba niseme KARIBUNI SANA.

Pamoja na kazi hii muhimu ya kukutambulisha wageni tulioungana nao leo,kwa idhini yako naomba nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi chimbuko la maadhimisho haya na shughuli mbalimbali ambazo tumezifanya ikiwa ni mojawapo ya kampeni za kuhamasisha umuhimu wa kuzingatia masuala usalama na afya mahali pa kazi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;** Tanzania leo inaungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku ya afya na usalama mahali pa kazi, maadhimisho haya ambayo hufanyika kila mwaka, huandaliwa na Serikali kupitia Taasisi yake ya OSHA kwa kushirikiana na wadau wa utatu (tripartite) ambao ni Shirikishola Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Chama cha Waajiri Tanzania

(ATE) pamoja na Shirika la Kazi Duniani (ILO) ambapo kupitia vikao vyetu vya maandalizi tulijadili namna ya kuiadhimisha siku hii ambapo Kauli Mbiu ya mwaka huu iliyotolewa na Shirika la Kazi Duniani na kuboresha na OSHA ili iendane na mahitaji yetu kwasasa ni: **Athari za mabadiliko ya tabia nchi katika usalama na afya kazini; Sajili eneo la kazi OSHA katika harakati za kupunguza athari hizo.**

**Mhe. Mgeni Rasmi;** Wafanyakazi ni nyenzo muhimu sana katika kuleta maendeleo ya Taifa, Lakini maendeleo haya yanategemea sana mazingira ya kazi ambayo shughuli za kiuchumi zinafanyika. Wafanyakazi wenye afya bora katika mazingira salama wanauwezo mkubwa wa kuleta mapinduzi makubwa ya uchumi katika taifa lolote. Hivyo basi kwa muktadha huo siku hii ya leo inalengo la kukumbushana, kuelimishana na kuhamasishana kuhusu uwepo wa mazingira salama na yenye afya katika maeneo ya kazi ili kulinda nguvu kazi ya taifa pamoja na uwekezaji na hatimaye kukuza pato la taifa na kupata maendeleo tarajiwa.

**Mhe. Mgeni Rasmi;** Maadhimisho haya ambayo siku ya leo Dunia nzima inaadhimisha na kutafakari hali ya wafanyakazi sehemu za kazi, yalitokana na kilio cha wafanyakazi kudai mazingira salama sehemu za kazi ambapo kwa mara ya kwanza maandamano makubwa yalifanyika Tarehe kama ya leo, Aprili 28, 1996 katika Jiji la New York nchini Marekani.

Lengo likiwa ni kuwakumbuka wafanyakazi waliokuwa wamepoteza

maisha, waliopata  ajali, waliopata magonjwa kazi, ama kupata ulemavu wakiwa kazini na kwa wakati huo yalikuwa yakiratibiwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Duniani chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo Endelevu la Umoja wa Mataifa.

**Mhe. Mgeni Rasmi;**, Shirika  la Kazi Duniani (ILO) ambacho likiwa kama chombo cha kusimamia viwango vya kazi Duniani Mwaka 2003, liliunga mkono juhudi hizo za shirikisho la vyama vya wafanyakazi  katika kuadhimisha siku hii. Nakupendekeza maudhui yenye lengo la kuhamasisha uwepo wa mazingira salama sehemu za kazi Badala ya kuadhimisha  kwa kufanya maandamo, ya kuonesha huzuni, masikitiko, kuweka mashada ya maua ikiwemo kuwasha mishumaa kwa wapendwa wao kama njia ya kudai haki ya mazingira salama,  ikapendekezwa kuwa maadhimisho hayo yafanyike kwa kuhamasisha wafanyakazi, waajiri na umma kwa ujumla kufanya juhudi za makusudi katika kuzuia ajali, magonjwa na vifo miongoni mwa wafanyakazi.

**Mhe. Mgeni Rasmi;** Kuanzia Mwaka 2004,  Nchi yetu kama nchi Mwanachama wa shirika la Kazi Duniani tumekuwa tukishiriki siku hii muhimu yenye lengo la kulinda haki ya mfanyakazi, ili kuleta maendeleo ya Taifa, kwa kushirikiana na wadau wetu nchini ambao ni Chama cha waajiri Tanzania(ATE), Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini (TUCTA)  pamoja na Shirika la kazi Duniani (ILO).

**Mhe. Mgeni Rasmi**; napenda nikiri kwamba  pendekezo la ILO  la kuwataka wafanyakazi kubadili maudhui ya maadhimisho haya kwa

kulia, kuandamana, kuweka maua, n.k na ushauri wa kuzitaka nchi wanachama kuunga mkono juhudi za wafanyakazi kuwataka waajiri kuweka mifumo ya kuwalinda wafanyakazi dhidi ya viharishi sehemu za kazi ili kuwe na mazingira salama limekuwa na matokeo chanya kwakuwa kumekuwa na mwamko na mwitikio kutoka kwa waajiri,wafanyakazi na umma kwa ujumla kuhusiana na umuhimu wa Kulinda uwekezaji na nguvu kazi ya taifa.

**Mhe. Mgeni Rasmi;** masuala ya Afya na Usalama ni masuala mtambuka, kwa kuwa yanagusa sekta zote za uchumi na kwamba pamoja na kuwa ni takwa la kisheria, lakini kwasasa masuala haya yanaangaliwa zaidi katika mrengo wa haki za binadamu, na kiutu zaidi, kwa mantiki hiyo elimu na ushirikishwaji wa pande zote za utatu ni muhimu sana ili kufikia azma ya lengo la nane (8) la Maendeleo Endelevu ya Dunia (Sustainable Development Goals) linalotaka kuwe na maendeleo ya ukuaji wa uchumi unaozingatia uwepo wa ajira zenye staha kwa watu wote.

**Mhe. Mgeni Rasmi;** Kauli Mbiu ya mwaka huu ni **Athari za mabadiliko ya tabia nchi katika usalama na afya kazini;** ,

**Mhe. Mgeni Rasmi,** katika vikao vya maandalizi na wadau OSHA kama Mamlaka inayohusika na usimamizi wa masuala ya usalama na afya za wafanyakazi mahali pa kazi, tuliamua kutohoa kauli mbiu hiyo ikisisitiza usajili wa sehemu za kazi. **"*Athari za mabadiliko ya tabia nchi katika usalama na afya kazini; Sajili***

***eneo la kazi OSHA katika harakati za kupunguza athari hizo”***

Hii ni kwa kutambua kuwa manejiment ya kwanza ya udhibiti wa vihatarishi vya mahali pa kazi inaanzia kwenye utambuzi wa eneo la kazi., usajili huo unawezesha kujua shughuli ya kiuchumi inayotarajiwa kufanyika, wafanyakazi wangapi wataajiwa, nyenzo gani zitatumika au kemikali gani na itatengeneza vihatarishi gani ili tuweze kujua namna ya kushauri maeneo ya kazi usimikaji ya mifumo madhubuti ya kudhibiti vihararishi sehemu ya kazi husika.

**Mhe. Mgeni Rasmi,** naomba nieleze kwa kifupi uhusiano wa jinsi kihatarishi hiki cha mabadiliko ya tabia nchi kinavyoathiri wafanyakazi katika ulimwengu wa kazi hasa katika masuala ya Usalama na Afya. **Mhe. Mgeni Rasmi,** mabadiliko ya tabia nchi huwa na matokeo tofauti ikiwemo kupelekea ukame, mvua juu ya wastani ambazo zimekuwa zikisababisha mafuriko, kuongezeka kwa kina cha bahari pamoja na kupanda na kushuka kwa joto ambavyo vyote huathiri maisha ya mwanadamu katika nyanja mbali mbali, ikiwa ni pamoja na masuala ya Usalama na Afya mahali pa kazi ambapo mabadiliko hayo yamekuwa ni chanzo kimojawapo cha vihatarishi vya ajali, magonjwa na vifo katika sehemu za kazi.

**Mhe. Mgeni Rasmi;** kutokana na athari hizo ikiwemo joto, idadi kubwa ya wafanyakazi duniani hulazimika kufanya kazi katika mazingira ya jua na joto kali na hivyo kuwa katika hatari ya kupata magonjwa ya kansa, figo, magonjwa ya mfumo wa hewa pamoja na changamoto ya afya ya akili

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**, athari tunazozingumzia

zimethibitishwa na Shirika la Kazi Duniani, kupitia utafiti wao wa hivi karibuni ambao unaonesha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya nguvukazi ya duniani, ipo katika hatari ya kukumbwa na vihatarishi vya usalama na afya vitokanavyo na mabadiliko ya tabia nchi. Shirika la Kazi Duniani linakadiria kwamba wafanyakazi bilioni 2 na laki nne **(2,400,000,000**) kati ya jumla ya nguvukazi ya watu bilioni 3 na laki nne (**3, 400,000,000**) wapo katika hatari ya kukumbwa na joto kali katika baadhi ya majukumu yao ya kila siku jambo ambalo linaweza kuwapelekea kupata baadhi ya magonjwa niliyoyaainisha hapo juu.

**Mhe. Mgeni Rasmi;** Nchi yetu ni sehemu ya dunia na takwimu hizo za ILO zinatuhusu ambapo madhara hayo kama yalivyoanishwa na takwimu za ILO ambapo tunaona madhara yake ni makubwa sana. Hivyo, kama nchi tunahitajika kuchukua hatua za makusudi katika kukabiliana na athari hizo.

Aidha , tusipochukua hatua za haraka na makusudi katika kudhibiti athari za mabadiliko ya tabia nchi katika usalama na afya kwa wafanyakazi, gharama yake itakuwa kubwa katika ngazi ya mtu mmoja mmoja, sehemu za kazi, katika jamii na kwa Taifa kiujumla. Kimsingi athari tajwa, zitapelekea kudorora kwa shughuli za uzalishaji na hivyokuathiri uchumi wa nchi yetu na dunia kwa ujumla kutokana na kuathirika kwa nguvukazi inayotumika katika uzalishaji.

Hivyo, ni wakati muafaka sasa kwa wadau kuimarisha mifumo kukaa na kujadili namna ya kuweka mifumo ya kulinda nguvukazi kutokana na athari hizo za mabadiliko ya tabia nchi kama hatua za

muda mfupi. Aidha, tunao wajibu wa kuhamasisha wadau wote wa masuala ya Usalama na Afya kushiriki kikamilifu katika program mbali mbali za Kitaifa zinazolenga kuhifadhi mazingira kwa lengo la kuyakabili mabadiliko ya tabia nchi.

**Mhe. Mgeni Rasmi**; hivyo kampeni ya mwaka huu imejikita zaidi katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na ushirikishwaji katika ngazi zote za maamuzi wakiwemo wafanyakazi ili nao wawe sehemu ya maamuzi katika harakati za kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;** OSHA kama Taasisi ya Serikali yenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria na taratibu mbali mbali zilizowekwa na nchi kwa minajili ya kulinda nguvukazi ya Taifa, sambamba na kuhamasisha wadau kuchukua hatua nyingine za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, tumeona ni muhimu kuunganisha jitihada hizo na kampeni ya usajili wa sehemu za kazi katika Taasisi ya OSHA kama njia mojawapo ya kuwaleta pamoja waajiri na wafanyakazi na wadau wengine katika kampeni hiyo ya kidunia ya kuhamasisha uhifadhi wa mazingira pamoja na kuimarisha mifumo ya usalama na afya inayoweza kudhibiti athari za mabadiliko ya tabia nchi katika usalama na afya kazini.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;** katika kutekeleza hayo yote kwa mwaka huu wadau, wameazimia kutekeleza shughuli mbali mbali zinazolenga kuhamasisha utekelezaji wa **Sheria Na.5 ya Mwaka 2003 ya Usalama na Afya mahali pa kazi** kwa kufanya yafuatayo:

- Kufanya mafunzo mbalimbali ya Usalama na Afya kazini kwa makundi mbali mbali ya wajariamali wadogo, mama lishe, boda boda na watu wenye ulemavu.

- Kuandaa maonesho yanayolenga katika kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa Sheria na taratibu mbalimbali za usalama na afya katika sehemu za kazi.

- kutoa tuzo kwa waajiri wanaozingatia vyema viwango vya usalama na afya, ambao watatangazwa na kukabidhiwa zawadi katika hafla maalum itakayofanyika usiku wa Aprili 30.

- Bonanza la michezo miongoni wa waajiri na wafanyakazi kwa lengo la kuendelea kutoa hamasa juu ya uzingatiaji wa kanuni bora za usalama na afya kazini pamoja kujenga umoja na mshikamano miongoni mwa wadau wetu wote wa masuala ya Usalama na Afya mahali pa kazi.

- Kuandaa na kuendesha kliniki kubwa ya uchunguzi wa magonjwa yatokanayo na kazi, magonjwa yasiyoambukiza, magonjwa ya kawaida ikiwemo kansa na magonjwa ya akina mama pamoja na kutoa ushauri nasaha na upimaji wa hiyari wa VVU. Kliniki hiyo inaongozwa na Madaktari Bingwa kutoka katika hospitali mbalimbali nchini pamoja na Wakaguzi wa Afya wa OSHA.

Katika shughuli tajwa, takribani maeneo ya kazi **92** yameshiriki katika maonesho pamoja na wajasiriamali wadogo wapatao **50** ambapo kumekuwa na mwitikio mkubwa ukilinganisha na mwaka jana ambapo maeneo ya kazi yapatayo **68** tu ndiyo yaliyoshiriki. Aidha, kwa mwaka huu washiriki **150**, wameshiriki katika tuzo ikilingalishwa na washiriki **40** wa mwaka jana.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;** kubwa zaidi katika maadhimisho haya, nimafanikio tuliyoyapata katika utekelezaji wa mkakati wa sasa wa Taasisi yetu wa kuhakikisha kuwa tunaifikia sekta isiyo rasmi ambapo kwa mwaka huu tumetoa mafunzo ya Usalama na Afya katika sekta za madini, mama lishe, boda, viwanda vidogo ambapo jumla ya wajasiriamali wadogo wapatao **5,112**, katika maeneo mbalimbali ya Kanda za Kaskazini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kusini na pamoja na Kanda ya Pwani walifikiwa hususan mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Arusha, Lindi, Mtwara Geita na Dar es Salaam.

Vilevile, OSHA imetoa mafunzo kwa Wahariri wa Vyombo vya Habari mbali mbali nchini wapatao 60. Mafunzo hayo yalijikita

katika kuwajengea uelewa kuhusu **Sheria Na. 5 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003** pamoja vihatarishi vya usalama na afya wanavyokumbana navyo wanahabari katika kutekeleza majukumu yao.

**Mafunzo hayo yote kwa makundi tajwa yamegharamiwa na Serikali.**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**; kwa kuhitimisha ningependa kuwakumbusha waajiri, wafanyakazi na umma kwa ujumla kuendelea kutekeleza wajibu wao kuhusiana na uimarishaji wa mifumo ya usalama na afya katika maeneo ya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Usalama na Afya kazini ikiwemo kuhakikisha kwamba maeneo yao ya kazi yamesajiliwa na OSHA ili wataalam wetu waweze kuwafikia kwa ajili ya ukaguzi wa mifumo iliyosimikwa na kutoa ushauri kitaalam kuhusiana na usalama na afya mahali pa kazi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**; ningependa kutumia fursa hii kuushukuru uongozi wa Mkoa wa Arusha ukiongozwa na **Comrade Paul Makonda,** kwa ushirikiano waliotupatia sambamba na kukubali kuwa mwenyeji wa maadhimisho haya. Ni matumanini yangu kuwa imekuwa ni fursa nzuri kwa wakazi wa Jiji la Arusha kufanya biashara na kujifunza kutoka kwa washiriki waliotoka katika mikoa mbalimbali nchini kuhusiana na utekelezaji wa Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

Baada ya taarifa hii ya maadhimisho ya mwaka huu Mheshimiwa Mgeni Rasmi, naomba nikushukuru tena wewe binafsi na viongozi wote ulio ambatana nao. Aidha, shukrani hizi pia ziwaendee wadau wetu na washiriki wote wa maadhimisho haya.

Kwa niaba ya menejimenti nzima ya OSHA, tunapenda kuwawatakia maadhimisho mema.

# Asanteni kwa kunisikiliza